

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**



**TAARIFA KWA UMMA**

**USAJILI WA SIMU ZA MKONONI**

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inawajulisha wananchi kuwa kuanzia tarehe 1 Julai 2009 makampuni yote ya simu za mikononi yataanza kusajili wateja wao waliopo na wapya ili kuhakiki umiliki wa namba za simu wanazozitumia. Zoezi hili litaendelea kwa miezi sita hadi tarehe 31 Desemba 2009.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inawahimiza wananchi kufahamu na kuzingatia mambo yafuatayo ambavo yametayarishwa kwa mfumo wa maswali na majibu.

1. **Swali:** Kwa nini usajili namba ya simu?  
**Jibu:** Kwa ajili ya kukulinda wewe na namba yako dhidhi ya matumizi mabaya ya simu.
2. **Swali:** Kitambulisho cha aina gani kitahitajika wakati wa usajili?  
**Jibu:** Ili uweze kusajiliwa unahitaji kufika kwenye ofisi ya kampuni yako ya simu au wakala wake na moja ya vitambulisho vifuatavyo ambapo utawapatia kivuli chake:-
  - (i) Kitambulisho cha mpiga kura
  - (ii) Pasipoti
  - (iii) Kitambulisho cha mfuko wa pensheni
  - (iv) Leseni ya udereva
  - (v) Kitambulisho cha SACCOS
  - (vi) Kitambulisho cha benki
  - (vii) Kitambulisho cha ajira pamoja na barua ya mwajiri
  - (viii) Kitambulisho cha chuo cha elimu ya juu
  - (ix) Kitambulisho cha uanachama kwenye kilabu
  - (x) Barua ya serikali za mitaa ikiwa na picha, sahihi na muhuri
3. **Swali:** Nisipojisajili ifikapo tarehe 31Desemba, 2009 nini kitatokea?  
**Jibu:** Namba yako itafungwa ili usiweze kuitumia kwenye mtandao wa simu nchini Tanzania.
4. **Swali:** Nani na wapi ninaweza kusajili namba yangu ya simu?  
**Jibu:** Unaweza kusajiliwa na kampuni yako ya simu za mikononi au mawakala wao waliopo sehemu mbali mbali nchini.
5. **Swali:** namba ngapi za simu (simcard) ambazo ninaweza/ninaruhusiwa kusajili?  
**Jibu:** Idadi yoyote kadri utakavyo.
7. **Swali:** Kuna uhakika gani wa usiri wa taarifa zangu nitakazotoa kwa kampuni ya simu za mikononi au wakala wao?  
**Jibu:** Kampuni zote za simu nchini zinawajibika kwa mujibu wa sheria, kutunza taarifa za wateja wao ikiwa ni pamoja na taarifa za matumizi.
8. **Swali:** Taarifa zipi zinahitajika wakati wa usajili?  
**Jibu:** Tafadhali angalia mfaano wa fomuya usajili hapo chini:-

Imetolewa na

Mkurugenzi Mkuu  
**Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)**

# Fomu ya Usajili wa Mteja

## Customer Registration Form

Passport Size  
photo  
Picha

**COMPANY NAME**

**Namba ya msambazaji**

Vendors Code \_\_\_\_\_

**Jina la Kampuni ya simu**

Name of Phone Company \_\_\_\_\_

### MAELEZO YA MTEJA/ CUSTOMER INFORMATION

**Jina kamili**

Full Name \_\_\_\_\_

**Tarehe ya kuzaliwa**

Date of Birth \_\_\_\_/\_\_\_\_/\_\_\_\_

**Jinsia:**

Gender:

**Mwanaume**

Male

**Mwanamke**

Female

**Anwani**

Address \_\_\_\_\_

**Mkoa**

Region \_\_\_\_\_

**Wilaya**

District \_\_\_\_\_

**Namba ya simu**

Number \_\_\_\_\_

**Namba ya "Sim Card"**

SIM Serial \_\_\_\_\_

**Namba ya utambuzi wa simu**

IMEI/ ESN \_\_\_\_\_

### UTAMBULISHO/ IDENTIFICATION

**Namba ya kitambulisho**

ID No. \_\_\_\_\_

**Kimetolewa na**

Issued by \_\_\_\_\_

**Aina ya kitambulisho:**

Type of ID:

**Pasi ya kusafiria**

Passport

**Leseni ya udereva**

Driving Licence

**Kitambulisho cha kazi**

Company ID

**Kitambulisho cha mpiga kura**

Voters ID card

**Barua ya mtendaji**

Local government letter

**Vinginevyo**

Others \_\_\_\_\_

### MAWASILIANO MENGINE(Kama Yapo)/ OTHER CONTACTS (If available)

**Namba ya simu:**

Tel No. \_\_\_\_\_

**Anuani ya barua pepe**

email address \_\_\_\_\_

**Namba ya simu ya mkononi**

Mobile no. \_\_\_\_\_

**S.L.B**

P.o. Box \_\_\_\_\_

**"Nathibitisha kuwa maelezo niliyotoa hapo juu ni ukweli mtupu na nafahamu kwamba nitawajibika kwa matumizi mabaya ya laini na namba yangu"**

*"I confirm to the best of my knowledge that the information provided above is true and I understand that I will be responsible for misuse of my simcard and number"*

**Saini ya mteja**

Customer Signature \_\_\_\_\_

**Tarehe**

Date \_\_\_\_\_

**Amehudumiwa na:**

Attended by \_\_\_\_\_

**Sahihi**

Signature \_\_\_\_\_

**Tarehe**

Date \_\_\_\_\_

**Mahali**

Location \_\_\_\_\_